| | | |
|---|---|---|
| | **COOPERATIVE LAW AND REGULATION INITIATIVE**<br>**(CLARITY)**<br>**KISWAHILI VERSION** | |

# KANUNI ZA CLARITY KWA AJILI YA MAREKEBISHO YA SHERIA

**November 16,2007**

# KANUNI ZA CLARITY KWA AJILI YA MAREKEBISHO YA SHERIA

## Kanuni kuu za CLARITY

Kwa muda mrefu vuguvugu la Ushirika limekuwa likitumia kanuni za Ushirika kama chombo cha kuwaunganisha. Kuenea kwa shughuli za ushirika huko Ulaya katikati hadi mwishoni mwa miaka ya 1800 kulikuwa ni matokeo ya kuundwa na kusambazwa kwa kanuni za ushirika kulikofanywa na vyama vya British Rochdale Society of Equitable Pioneers (Chama cha Rochdale cha Uingereza cha Mapayonia wa Haki) na German Raiffeisen Savings and Credit Cooperative (Chama cha Kuweka na Kukopa cha German Raiffeisn) Kanuni zilizokuwa zikitumiwa na vyama hivi baadaye ziliboreshwa na Umoja wa Ushirika wa Kimataifa (ICA) na Shirika la kazi Duniani (ILO) kwa ajili ya kuendeleza vyama vya Ushirika katika nchi zinazoendelea. Ingawa msingi wake ni huu pamoja na jitihada nyingine za kufafanua kanuni za shughuli za vyama vya ushirika, CLARITY ni ya pekee katika uundaji wake wa kanuni mahsusi na zinazoeleweka kwa kuchambua mazingira ya kisheria na udhibiti.

Baadhi ya kanuni za CLARITY zinatokana na kanuni na shughuli za ushirika zilizodumu kwa muda mrefu. Hasa, kanuni inayosema kwamba vyama vya ushirika lazima vitegemee udhibiti wa kidemokrasia kwa uwanachama, na viwe huru na visitegemee serikali, wala watu au vyombo vingine mbali na wanachama wa ushirika. Hii ilikuwa kanuni ya msingi ya Rochdale na matamko mengine ya maadili ya ushirika. Lakini kanuni hii mara kwa mara ilikuwa haipewi umuhimu katika mifumo ya kisheria ya nchi zinazoendelea.

Kama ilivyoelezwa kwenye Kiambatisho A, hapo awali kulikuwa na dhana yenye nguvu miongoni mwa wataalamu na maofisa wa Serikali kwamba vyama vya ushirika katika nchi zinazoendelea vilihitaji kuongozwa na serikali ili viweze kuendelea. Fikra hizi zilitumika kuhalalisha kuondolewa kwa misingi ya demokrasia katika uendeshaji wa ushirika na kutoa nafasi kwa maafisa wa Serikali na viongozi kuongoza na kudhibiti shughuli za ushirika. Mtazamo huo sasa umebadilika. Mtazamo unaokubaliwa zaidi kwa sasa na mtazamo wa dhati wa CLARITY, ni kwamba udhibiti wa Serikali kwa vyama vya ushirika unaleta madhara zaidi kuliko faida na kwamba vyama vyote vya ushirika, bila kujali ngazi zao za maendeleo au nchi zao za asili, vinapaswa kuwa na haki ya kuongoza shughuli zao wenyewe kidemokrasia na kwa uhuru.

Kanuni nne za mwanzo za CLARITY zinatokana na umuhimu wa kuwa na sheria za kulinda na kuendeleza udhibiti wa kidemokrasia wa vyama vya ushirika kwa uanachama. Kanuni za CLARITY zinathibitisha kuwa mifumo ya kisheria na kikanuni zinapaswa:

- Kulinda mfumo wa kidemokrasia wa vyama vya ushirika, kukabidhi udhibiti wa chama kwa wanachama wake.
- Kulinda uhuru wa vyama vya ushirika katika uendeshaji bila ya kuingiliwa na watu wa serikali, au vyombo vingine ambavyo sio wanachama wa ushirika.
- Kulinda uhiyari wa uanachama katika vyama vya ushirika, kuruhusu uwanachama uamuliwe na ushirika wenyewe, na sio kuamriwa na sheria au agizo la serikali; na
- Kulinda na kuendeleza dhima za uanachama zikijumuisha majukumu ya kuchangia na kuthibiti mtaji wa ushirika kwa usawa na kidemokrasia.

Kanuni mbili zinazofuata za CLARITY za kisheria na kikanuni zinalenga kutazama uhusiano baina ya vyama vya ushirika na shughuli nyingine ndani ya uchumi. Pale ambapo Serikali inatoa mwongozo na kusimamia vugu vugu la maendeleo ya ushirika, vyama vya ushirika vimekuwa vikikatazwa kujiingiza katika baadhi ya shughuli za biashara na udikteta wa kiutawala wa sheria au agizo la serikali. Zaidi ya hayo, mifumo

ya kikanuni, ikiwemo ile iliyowekwa kuendeleza ubinafsishaji wa viwanda, mara nyingi hubagua ushiriki wa vyama vya ushirika kwa kutumia masharti magumu yanayolenga kunufaisha biashara (makapuni) makubwa au mashirka makubwa ya kiserekali na kikiritimba.

Ili kuimarisha haki sawa kwa vyama vya ushirika, kanuni za CLARITY zinashauri kwamba mifumo ya kisheria na kikanuni vinapaswa:

- ❖ Kusiwe na upendeleo mkubwa kwa vyama vya ushirika zaidi ya aina nyingine za biashara zilizomo kwenye sekta hiyo hiyo, na wakati huo huo kulinda na kuwa na wepesi wa kuona mabadiliko ya pamoja ya vyama vya ushirika; na
- ❖ Kutoa nafasi na vivutio vinavyofaa, kila vitakapohitajika, ili kuwezesha aina zote za shughuli za ushirika kuendeshwa ndani ya sekta.

---

*Mara nyingi vyama vya ushirika vinasajiliwa, kuongozwa na kuwa na mielekeo ya kuwa katika mchakato wa kusuluhisha migogoro katika wakala huohuo, na kusababisha mwingiliano na migongano ya maslahi katika shughuli/kazi mbalimbali.*

---

Kanuni tatu za mwisho za CLARITY zinahusu muundo wa kitaasisi na utendaji wa mfumo rekebishi. Katika nchi nyingi, kuanzishwa kwa mfumo tofauti na wa kipekee ya usajili na usimamizi wa ushirika kumepelekea kukosa ufanisi na utaratibu usio wa haki na ambao biashara nyingine binafsi hazikabiliwi nazo. Kwa mfano, vyama vingi vya ushirika lazima vipate idhini ya ukubalifu ya kufanya kazi kutoka kwa mrajisi wa vyama vya ushirika au lazima watimize muda wa kusubiri ulioamriwa kisheria, ingawaje aina nyingine za biashara zinaidhinishwa kwa kukisiwa na mpaka labda msajili wa makampuni atakapoamua vinginevyo. Mara nyingi vyama vya ushirika vinasajiliwa, kuongozwa na kuwa na mielekeo ya kuwa katika mchakato wa kusuluhisha migogoro katika wakala huohuo, na kusababisha mwingiliano na migongano ya maslahi katika shughuli/kazi mbalimbali.

Ili kupunguza kasoro za kisheria ambazo zinaweza kufifisha maendeleo ya ushirika, na kutoa huduma sawa kwa vyama vya ushirika dhidi ya aina nyingine za biashara, kanuni za CLARITY zinaonya kwamba mifumo ya kisheria na kikanuni inapaswa:

- ❖ Iwe rahisi, inayobashirika na yenye ufanisi, kupunguza ucheleweshaji wa kirasimu na vikwazo katika uendeshaji wa shughuli, na inapaswa kuepuka migogoro na urudufu wa sheria nyingine;
- ❖ Kukubaliana na mchakato wa kisheria, zikiwemo haki zinazotumika za kusikilizwa, uwakilishi, na rufaa zisizo na upendeleo, kwa ajili ya maamuzi ya dola ambayo yanagonganisha vyama vya ushirika au wanachama wake; na
- ❖ Kusimamia wajibu wa serikali katika utekelezaji wa sheria, utatuzi wa migogoro, leseni, na uimarishaji kwa namna ambayo inaepusha urudufu, ushawishi usiostahili, na kupunguza migongano ya maslahi.

Kila mojawapo ya kanuni hizi kuu zilizoelezwa hapo juu zimedhamiriwa kuwa za mjumuisho na kwamba CLARITY haijaidhiisha lugha ya kisheria ambayo inaamini kwamba inapaswa kutumiwa katika muktadha fulani. Kanuni hizi zimebuniwa kuusaidia vuguvugu la ushirika kuchunguza lugha mahsusi ya kisheria au utekelezaji wa kanuni na kuona kama vinalinda na kuendeleza ipasavyo mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo ya ushirika. Utengenezaji rasimu wa lugha mahususi ya kisheria umeachwa kwa ajili ya mchakato wa ndani.

## Kanuni kuu za CLARITY kwa ajili ya Mazingira Wezeshi ya Kisheria na Kikanuni

- **Kulinda udhibiti wa kidemokrasia wa mwanachama**: Sheria lazima ilinde sifa ya kidemokrasia ya vyama vya ushirika, kwa kukabidhi udhibiti wa chama kwa wanachama wake.
- **Kulinda uhuru**: Vyama vya ushirika ni shughuli za sekta binafsi. Sheria lazima ilinde uhuru wa vyama vya ushirika katiaka kufanya maamuzi bila ya kuingiliwa na serikali, watu au vyombo vingine visivyo wanachama wa ushirika.
- **Kuheshimu uanachama wa hiari**: Sheria lazima ilinde hali ya uwanachama wa hiari katika vyama vya ushirika; uwanachama katika vyama vya ushirika unapaswa kuamuliwa na kila ushirika, sio kuamriwa na sheria au agizo la serikali.
- **Ushiriki wa mwanachama katika shughuli za uchumi**: Sheria lazima ilinde na kuendeleza majukumu ya uanachama, yakiwa ni pamoja na wajibu wa kuchangia kwa usawa na kudhibiti kidemokrasia mtaji wa ushirika.
- **Kuhamasisha usawa katika huduma:** Kusiwe na upendeleo mkubwa kwa vyama vya ushirika zaidi ya aina nyingine za biashara zilizomo kwenye sekta hiyo hiyo, na wakati huo huo kulinda na kuwa na wepesi wa kuona mabadiliko ya pamoja ya vyama vya ushirika. Usajiri, utekelezaji wa sheria, utatuzi wa migogoro na utoaji leseni kwa vyama vya ushirika unapaswa kushughulikiwa kama zinavyoshughulikiwa aina nyingine za biashara.
- **Kuimarisha ufikiaji wa masoko**: Kanuni mahsusi za kisekta zinapaswa kutoa nafasi na vivutio vinavyofaa, kila vitakapohitajika, kuwezesha biashara za ushirika kufanya kazi.
- **Kutoa mfumo rekebishi unaofaa na wa ufanisi:** Mfumo wa usimamizi unapaswa kuwa rahisi, unaobashirika, na wenye ufanisi, unapaswa kupunguza ucheleweshaji wa kirasimu na vikwazo katika uendeshaji wa biashara; na unapaswa kuepuka migogoro na urudufu wa sheria nyingine. Kanuni zinazohusu shughuli ya vyama vya ushirika zinapaswa kushughulikiwa na taasisi zenye utaalamu mkubwa unaofaa.
- **Kulinda mchakato unaostahili**: Vyama vya ushirika na wanachama wake vinapaswa kukubaliwa kwenye mchakato wa sheria, ukijumuisha haki zinazotumika za kusikilizwa, uwakilishi, rufaa zisizo na upendeleo, kwa ajili ya maamuzi serikali ambayo huathiri vyama vya ushirika au wanachama wake.
- **Kuepuka Migongano ya Maslahi**; Wajibu wa serikali katika utekelezaji wa sheria, utatuzi wa migogoro, leseni, na uendelezaji vifanywe kwa namna ambayo vinaepuka urudufu, ushawishi usiofaa, na kupunguza migongano ya maslahi.

## Mifumo ya kichanganuzi ya CLARITY

Kuonyesha jinsi kanuni za CLARITY zinavyoweza kutumika kutathmini mazingira ya kisheria na kikanuni, CLARITY ilitayarisha mifumo miwili ya kichanganuzi ya kutumiwa na vyama vya ushirika na watetezi wengine wa sera. CLARITY ilikusanya na kupitia idadi kubwa ya sheria za ushirika na kufanya tafiti kuhusu utekelezaji wa kanuni kwenye ushirika katika nchi nyingi ambako wanachama wake wengi wanafanya kazi. Kutokana na utafiti huu, mradi ulianzisha mifumo miwili, mmoja ukilenga vipengele vya pamoja vya sheria na taratibu mahsusi za ushirika, mwingine ukilenga vipenegele vya kawaida katika kanuni mahususi za kisekta ambazo huathiri ushiriki katika ushirika.

Katika kila mfumo, CLARITY inabainisha kwa nini na ni vipi moja au zaidi ya kanuni kuu huweza kutumika kwa kipengee mahususi cha mfumo wa kikanuni. Maoni kuhusu

taratibu ambazo zitaweza kutekeleza kanuni kwa mafanikio zimejumuishwa katika kila mfumo, pamoja na ubainishaji wa sababu za umuhimu wa eneo hilo la sheria na kanuni rekebishi kwa maendeleo ya ushirika. Mifano maalum ya vitendo vya kuwezesha au kudhoofisha zinazotokana na sheria kanuni rekebishi za zamani na za sasa zinajumuishwa ili kuzilinganisha.

Mifumo hii sio sheria za mfano. Hazijakusudiwa kuonyesha lugha au vipengee vya mfano ambayo yanapaswa kufuatwa katika kila nchi. Badala yake, mifumo inakusudiwa kuonyesha jinsi kanuni za CLARITY zinavyoweza kutumika kuchambua mazingira mahususi ya mijadala ya kikanuni na inayohitaji mabadiliko ya kikanuni. Habari zaidi juu ya hili zinapatikana kwenye viambatisho
Mwishon mwa ripoti hii nakwenytovuti ya CLARITY.
www.ocdc.coop/clarity/default.htm.

## KANUNI ZA USHIRIKA YA KISHERIA NA UDHIBITI

### 1. Uundaji na Usajili wa Ushirika

| Kanuni kuu | Utekelezaji wa Kanuni Kuu | Sababu za Msingi |
|---|---|---|
| Kuwe na mfumo wa kikanuni ulio wazi na unaofaa | Muda ambao usajili unatakiwa uwe umefanyika. Kupunguza uwezekano wa vipindi virefu vya ucheleweshaji wa kirasimu, muda unaweza kupangwa ambapo uidhinishaji wa maombi ya usajili ambapo baada ya muda huo maombi yatachukuliwa kuwa yamepitishwa | Katika nchi ambako michakato wa usajili ina usumbufu, haifanywi kwa wakati au isiyo na uhakika kwa uhakika, mara nyingi vyama vya ushirika hujisajili chini ya sheria za mashirika yasiyo ya kiserikali na makampuni |

**Mfano mzuri na wezeshi: Sheria ya vyama vya ushirika ya Philippines, 16, 1990:** "*Maombi yote ya usajili yatakuwa yamefanyiwa kazi... ndani ya kipindi cha siku thelathini (30).... vinginevyo maombi yatachukuliwa kuwa yamekubaliwa*".

**Mfano mbaya na usio wezeshi: Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Ghana, 1968**: Sheria inaamuru muda wa miezi sita wa majaribio kwa ajili ya uandikishaji wa vyama vya ushirika ambao mara nyingi huongezwa hadi miaka miwili au zaidi.

| | | |
|---|---|---|
| Kuhamasisha usawa katika huduma | Sajili vyama vya ushirika katika ofisi zile zile zinazosajili aina nyingine za biashara. Ikiwezekana weka shughuli za usajili kwenye taasisi moja na zile zinazosajili aina nyingine za biashara. | Vyama vya ushirika vishawishiwe kutokutumia michakato ya usajili ambayo ni migumu zaidi ya ile inayotumiwa na aina nyingine za biashara. |

**Mfano mzuri na wezeshi: Marekani:** Kanuni za ushirikishaji/maombi ya uandikishwaji huwasilishwa kwa mujibu wa Sheria za kawaida za usajili wa Makampuni na zinachukuliwa kuwa ushahidi tosha wa kuwa ushirika husika umesajiliwa kwa mujibu wa Sheria.

| | | |
|---|---|---|
| Kuepuka mgongano wa kimaslahi | Orodhesha Kazi na majukumu ya Mrajisi: Pale ambapo kunakuwa na mrajisi mahsusi kwa ajili ya vyama vya ushirika, basi majukumu yake yawekwe bayana ili kuondoa majukumu mengine yasiyo ya kiusajili kama ya ustawi, usimamizi, na utatuzi wa migogoro. | Kuchanganya kazi za uthibiti na ustawishaji katika ofisi moja kunasababisha migongano ya asili ya maslahi ambao unahatarisha dhana ya kutoingiliana kati ya usajiri, usimamizi na shughuri za ustawishaji |

**Mfano mzuri na wezeshi:** **Afrika ya Kusini** : Ilihamisha urajisi wa vyama vya ushirika kutoka Wizara ya Kilimo kwenda Wizara ya Biashara ili kutenganisha majukumu maalumu ya uhamasishaji na uendelezaji kisekta kutoka kwenye kazi ya urajisi.

**Mfano mbaya na usio wezeshi:** **Sheria ya Vyama vya Ushirika wa mikopo ya India, 1904:** Muundo wa utungaji wa sheria za vyama vya ushirika ulioigwa toka Uingereza "*The Classical British India*" unasababisha migongano ya asili ya maslahi kwenye ofisi ya mrajisi kwa kuikabidhi ofisi majukumu yote mawili ya udhibiti na ustawishaji

| | | |
|---|---|---|
| Kulinda kujitegemea na uhuru wa kufanya maamuzi | Kuepuka ulazima wa kuwa na mfano fulani ya sheria ndogondogo katika ushirika. Mchakato na sheria za usajili zinapaswa kuwa na uwezo mkubwa wa kubadilika kwa urahisi kwa ajili ya ushirika kuelezea utawala wake kupitia sheria ndogondogo na katiba ya ushirika | Msingi wa mafanikio ya vyama vya ushirika ni kukua kwa uwezo wa wanachama wake wa kuongoza chama kidemokrasia na kufuata muundo wenye manufaa zaidi kwa mujibu wa shughuli zake |

**Mfano Wezeshi:** **Botswana, Sheria ya Vyama vya Ushirika ξ 125, Nyongeza 1, 1989:** Sheria inatoa mahitaji ya chini kabisa kwa sheria ndogondogo kama vile kujumuisha taratibu za kuteua na kuachisha kazi maofisa, bila ya kuamrisha lugha maalum.

**Mfano Usio wezeshi:** **Sheria ya 1968 ya Vyama vya Ushirika ya Thailand**: Mara nyingi Msajili anaweka sheria ndogondogo za kielezo kuhusu vyama vya ushirika.

### 2. Usimamizi wa Ushirika

| Kanuni Muhimu | Utekelezaji wa Kanuni Kuu | Kanuni za Msingi |
|---|---|---|
| Kuendeleza utendaji uliosawa<br>Kulinda uhuru wa kujitawala | Utaratibu wa kuratibu shughuli za biashara. Nchi nyingi hujumuisha shughuli za uongozaji katika mamlaka zinazohusika na kushughulikia shughuli nyingine | Vyama vya ushirika vinapaswa kuongozwa na taratibu za usimamizi kma zilizo katika shughuri nyingine. Taratibu kuu za usimamizi kwa ajili ya vyama vya ushirika zinapaswa kuwa na lengo la kuwapa wanachama uwezo wa kuongoza chama |

**Mfano Wezeshi:** **Kanuni za Ushirika za Ufilipino, ξ 124 (2), 1990**: Kupiga marufuku "kuingilia moja kwa moja au kusiko kwa moja kwa moja kwa kiongozi au mwajiriwa yeyote wa serikali kwenye masuala ya ndani ya ushirika ambako sio mwanachama."

**Mfano usio Wezeshi:** **Waraka rasmi wa Serikali ya Uganda wa 1968 kuhusu Masuala ya Vyama vya Ushirika:** Wajibu wa Serikali ni kusaidia na kuelekeza (Vyama vya Ushirika) katika uhusiano huu serikali inakusudia kuufanya udhibiti wa chama cha ushirika moja kwa moja kuwa chini ya udhibiti wa Waziri.

| | | |
|---|---|---|
| Kuepuka mgongano wa Wajibati | **Kutenganisha shughuli za udhibiti na shughuli za kiuendelezaji**. shughuli za udhibiti zinapaswa kutenganishwa na shughuli nyingine kisheria, kama vile uendelezaji au usajili. | Kuweka katika chombo kimoja majukumu yote mawili ya uhamasishaji na utekelezaji wa sheria unaweza kusababisha migongano ya wajibati ambayo itahatarisha ufanisi na uhalali wa kanuni |

***Mfano Wezeshi:* Mswada wa 4 ξ 75, ξ 80,2006 wa Vyama vya Ushirika wa Afrika ya Kusini.**

Bodi ya Ushauri ya Ushirika hushauri serikali na kutoa mapendekezo kuhusiana na sera, lakini inakosa dhima ya kikanuni ya moja kwa moja juu ya vyama vya ushirika.

***Mfano Usio Wezeshi:* Sheria ξ ya 3, 1990 ya Mamlaka ya Maendeleo ya Ushirika ya Filipino:**

Mamlaka ya Maendeleo ya Ushirika hupewa mamlaka yote ya usajili, uendelezaji na kanuni za vyama vya ushirika.

### *3. Hadhi na Haki za Kisheria*

| **Kanuni Kuu** | **Utekelezaji Kanuni Kuu** | **Sababu za Msingi** |
|---|---|---|
| Kukuza utendaji uliosawa<br><br>Kulinda uhuru na uwezo wakujitawala na kufanya maamuzi | Utu wa kisheria. Ushirika unapaswa kuwa na utu wa kisheria sawa na ule uliopo katika Makampuni. Kwa mfano, vyama vya ushirika vinapaswa kuwa na haki kamili ya kumiliki mali, kuingia mikataba, kushtaki, au kushtakiwa | Kwa ujumla Kampuni iliyosajiriwa, kishria ina nguvu kama za mtu binafsi ili kuwa na nguvu kama alizonazo mtu binafsi katika kumiliki mali, kuingia mikataba na kushtaki au kushtakiwa. Utu wa kisheria ni miongoni mwa vitu muhimu katika kuanzisha na ushirika kama chombo kinachojitegemea mbali na Serikali. muhimu katika kuanzisha vyama vya ushirika kama vyombo binafsi kuhusiana na serikali. |

*Mfano Wezeshi*: **Sheria ya Ushirika ya Ukraine, ξ 23,2003:** “Vyama vya Ushirika vinastahili kufanya kila shughuli zilizoonyeshwa kwenye sheria zao ambazo hazikatazwi na sheria.”

| | | |
|---|---|---|
| Kuhamasisha utendaji ulio sawa | Deni/ kuwafidia maofisa na Wakurugenzi, kama ilivyo kwa viongozi wengine, wakurugenzi na maofisa wa ushirika wanapaswa kulipwa fidia na ushirika wanaposhtakiwa kutokana na majukumu yao kwenye ushirika, labda deni hilo liwe limetokana na kushinda kwa makusudi au kiuzembe kutekeleza kwa uaminifu majukumu | Vyama vya ushirika au viongozi wake hawapaswi kujihami kutokana na sheria zinazotumika kwa ujumla. Kuhakikisha kunakuwepo na uwajibikaji wa viongozi kwa ushirika. Viongozi hao wanapaswa kuwa na wajibu wa kuaminika unaotekelezwa |

| | | |
|---|---|---|
| | waliyokabidhiwa na ushirika | na viongozi wa ushirika. |

**Mfano Wezeshi:**
**Mswada 4, ξ 75, ξ 37 (1), 2005 wa Vyama vya Ushirika wa Afrika ya Kusini**: Wakurugenzi, mameneja na wafanyakazi hawawajibiki na hatua zozote zinazochukuliwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kama hazihusishi mwenendo mbaya wa makusudi, kukosa uaminifu, uzembe wa hali ya juu au tabia ya kutokujali.

**Mfano usio Wezeshi:** **Sheria ξ 6 (a), 2003 ya Vyama vya ushirika Vya Sudani**: kwa madhumuni ya dhima ya kijinai, mali ya ushirika itachukuliwa kuwa ni mali ya umma na wafanyakazi wake watachukuliwa kuwa ni watumishi wa umma.

### 4. Uwanachama

| **Kanuni Kuu** | **Utekelezaji wa Kanuni Kuu** | **Sababu za Msingi** |
|---|---|---|
| Kuheshimu uwanachama wa hiari | Hakuna uwanachama wa kulazimishwa. Serikali haipaswi kuwa na mamlaka ya kulazimisha uwanachama kwenye ushirika | Uwanachama wa kuamriwa na serikali unaondoa sifa ya kidemokrasi ya chama cha ushirika na kiuharibu uhusiano wa kiuwajibikaji kati ya ushirika na wanachama wake |

**Mfano Wezeshi:**
**Mswada 4, ξ 75, ξ 3 (1) (a), 2005 wa Vyama vya Ushirika vya Afrika ya Kusini:** Vyama vya ushirika vinachukuliwa kuwa vimefuata kanuni za ushirika "endapo uwanachama wa ushirika huo ni wazi kwa watu ambao wanaweza kutumia huduma za ushirika huo na ambao wako tayari na wanaweza kuyakubali majukumu ya uwanachama."

**Sheria ξ 5, 2003 ya Jumla ya Vyama vya Ushirika vya Bosnia**: Inatamka kwamba wanaume na wanawake watendewe sawa kuhusiana na uwanachama katika vyama vya ushirika.

**Mfano usio wezeshi**
***Misri, 1952*:** Serikali inaamrisha kwamba wakulima katika sekta fulani waungane wa vyama vya ushirika vinavyoshughulikia kilimo.

**Zambia, Sheria ya ξ 3, 1970 ya Vyama vya Ushirika:** "Serikali ina uhuru wa kuchukua hatua za kiushauri kama inavyoona, kutia moyo maendeleo ya ushirika" unatumiwa kutwaa shughuli za masoko ya kilimo na kuamrisha uwanachama katika vyama vya ushirika.

| | | |
|---|---|---|
| Kulinda udhibiti wa uwanachama wa kidemokrasia | **Uhuru wa kupanga ukubwa na sifa za uwanachama.** Vyama vya ushirika vinapaswa kuamua kupitia taratibu za utawala wa ndani mahitaji ya ukubwa na vigezo vya kustahili uwanachama, kulingana na sheria zinazotumika kwa ujumla zisizo za kibaguzi | Idadi na ofisi za wanachama kuunda ushirika zitatofautiana. Ni wajibu wa wanachama na uongozi kuamua sifa za uwanachama ambazo zitahakikisha yanakuwepo mafanikio ya mradi. |

**Mfano Wezeshi:**
**Sheria ya Raia Na. 10406, Kifungu cha 11, ξ 1094, 2002 ya Brazil**: Inaruhusu vyama vya ushirika kuwa na idadi ndogo ya wanachama wanaotegemea mahitaji ya uongozi ya vyama vya ushirika.

**Mfano usio Wezeshi:**
**Sheria ξ 12 (i), 2003** ya Vyama vya Ushirika vya Sudani. Wanachama wa vyama vya msingi hawatakuwa pungufu ya watu 20. Msajili anaweza kupanga idadi ndogo ya wanachama katika chama katika masuala maalum kwa ajili ya uzingativu wa kijamii na kijiografia."

**Sheria ξ 11,2003 ya Ushirika ya Ukraine:**Inahitaji malipo ya ada ya kiingilio ya kujiunga na ushirika.

| | | |
|---|---|---|
| Kulinda Uhuru na kujitawala | Kupiga marufuku Sheria ya ushirika. Haipaswi kuiruhusu serikali kuwa mwanachama wa ushirika | Ushiriki wa serikali kwenye uwanachama wa ushirika unaondoa dhima ya biashara kama asasi binafsi isiyofahamika |

**Mfano Wezeshi:**
**Kanuni ξ 28, 1990 ya Ushirika wa Filipino**: Ofisa au mfanyakazi yoyote wa Mamlaka ya Maendeleo ya Ushirika, au kiongozi yeyote wa serikali aliyechaguliwa, hastahili kuwa ofisa au mkurugenzi wa ushirika.

**Mfano usio Wezeshi.**
**Sheria ya mwaka 1925 ya Vyama vya Ushirika ya India Bombay:** Inaiidhinisha serikali kushiriki kwenye mtaji wa hisa wa vyama vya ushirika.

## 5. Utawala kwa Wanachama

| Kanuni Kuu | Utekelezaji wa Kanuni Kuu | Sababu za Msingi |
|---|---|---|
| Kulinda udhibiti wa kidemokrasia wa mwanachama | **Kanuni ya kura ya wengi**. Sheria ya ushirika inapaswa kuruhusu sheria ndogondogo za ushirika kutekeleza kanuni za upigaji kura ambazo zinalingana mahitaji ya uongozi/utawala wa kidemokraisa ikiwa ni pamoja na mtu mmoja kura moja, uamuzi wa wengi wa kubadilisha muundo wa ushirika, kura za kulimbikiza na mahitaji ya mamlaka ya kuteua watu wa kupiga kura | Vyama vya ushirika vinapaswa kuongozwa kidemokrasia, lakini kwa kupewa uwezo wa kufafanua taratibu kidemokrasia ndani ya chama |

**Mifano Wezeshi:** **Mswada 4, ξ 75, ξ 3 (1) (b), 2005 wa Vyama vya Ushirika Afrika ya Kusini:** Kwa vyama vya Ushirika vya Msingi, kila mwanachama ana kura moja."

**Mifano Usio Wezeshi:**
**Hungary:** Sheria maamuzi mengi kwa misingi ya uwingi wa kura moja tu

**Sheria ξ 30, 2003 ya Vyama vya Ushirika ya Bosnia:** Inaruhusu haki ya kupiga kura kupimwa kulingana na mchango wa kila mtu kwenye ushirika.

| | | |
|---|---|---|
| Kulinda udhibiti wa kidemokrasia wa mwanachama | Nafasi ya kukagua kumbukumbu. Kuwezesha udhibiti wa mwanachama katika uongozi, kumbukumbu za biashara kwa ujumla zinapaswa kuwa wazi kwa ajili ya kukaguliwa na kila mwanachama wa ushirika | Wanachama wa Ushirika wana jukumu la usimamizi wa bodi ya wakurugenzi na wanapaswa kujulisha na kupewa taarifa za kutosha ili watekeleze vema kazi hiyo. |

**Mfano Wezeshi:**
**Sheria ξ 27 (b) ya Ushirika ya Mongolia, isiyo na tarehe:** Bodi ya wakurugenzi inahusika na utunzaji wa kumbukumbu/rekodi, kuifahamisha bodi ya ukaguzi wa hesabu kuhusu kupokelewa kwa taarifa ya mwaka, na kuwasilisha taarifa hiyo kwa wanachama.

**Sheria ξ 12,2003 ya Ushirika ya Ukraine:**
Wanachama wana haki ya kuomba "taarifa kuhusu uwanachama kwenye ushirika, uendeshaji wa ushirika na viongozi wake.

## 6. Maofisa na Wakurugenzi

| **Kanuni Kuu** | **Utekelezaji wa Kanuni Kuu** | **Sababu za Msingi** |
|---|---|---|
| Kulinda uhuru wa kufanya maamuzi na kujitawala | Epuka tafsiri za kina za kazi za Uongozi. Sheria ya Ushirika inaweza kutoa maelekezo ya jumla kuhusu mgawanyo maalumu wa majukumu kati ya bodi ya wakurugenzi na menejimenti bila ya kueleza kwa kina kwa ajili ya kuzuia unyumbufu katika kupanga biashara. | Muundo wa uongozi wa ushirika unapasswa kuakisi mkabala unaofaa kwa ajili ya sekta ya ushirika huo na uwezo wa kiuendeshaji. Miundo ya jumla inaweza isifae kwa ushirika mwingine |

**Mfano Wezeshi:** **Sheria ξ 23 ya Ushirika ya Mongolia: haikuwekwa tarehe:** Wanachama walio wengi huchagua bodi ya uongozi, bodi ya ukaguzi wa hesabu na wakurugenzi, na kupanga majukumu yao

| | | |
|---|---|---|
| Kulinda uhuru | Hakuna uteuzi wa mameneja utakaofanywa na serikali. Serikali haipaswi kuwa na haki yoyote ya kuteua mameneja wa ushirika | Ushirika unategemea uhusiano muhimu wa uwajibikaji baina ya wanachama na viongozi waliochaguliwa, na sio baina ya viongozi wa ushirika na serikali |

**Mifano Wezeshi:** **Marekani (U.S.A), Jimbo la Wisconsin. Ξ 185.35, 2004:** Maofisa wote watakuwa na mamlaka na kutenda kazi kama zitakavyotolewa na sheria ndogo ndogo au kama bodi itakavyoona kwamba hazilingani na sheria ndogondogo.

**Mfano usio Wezeshi: Sheria ξ 161 (1), 1970 ya Vyama vya Ushirika ya Zambia**: Inampa Msajili madaraka ya kuteua ofisa mmoja au zaidi wa kusimamia masuala ya chama."

| | | |
|---|---|---|
| **Kulinda uhuru** | **Usimamizi Huru wa fedha**. Kwa mujibu wa mahitaji ya ukaguzi wa hesabu ya jumla, vyama vya ushirika vinapaswa kuwa makini na matumizi na vitega uchumi vyao. Sheria haipaswi kuamuru kuhusu matumizi kwa shughuli mahususi au kuhitaji idhini ya serikali ya uamuzi wa msingi wa biashara | Uhuru katika usimamizi ni sifa kuu ya shughuli binafsi. Vyama vya ushirika lazima vijifunze juu ya shughuli zenye mafanikio/ufanisi kwa kujisimamia, sio ulinzi mkubwa wa serikali |

**Mfano Wezeshi:** **Kanuni za Ushirika ξ 9, 1990 za Ufilipino**:zinavipa vyama vya ushirika mamlaka ya kupangisha, kuweka rehani, kununua, na kufanya shughuli nyingine zozote maadamu shaughuri hizo zimetajwa katika katiba na mwongozo wa vyama hivyo.

**Mfano usio Wezeshi:** **Sheria ya 1970 ya Vyama vya Ushirika ya Zambia:** Msajili ana mamlaka ya kuidhinisha shughuli nyingi za usimamizi, zikiwa ni pamoja na kukopa, kuwekeza katika hisa na amana, kutumia raslimali za chama na shughuli za ukodishaji.

## 7. Bodi ya Wakurugenzi

| **Kanuni Kuu** | **Kutekeleza Kanuni Kuu** | **Sababu za Msingi** |
|---|---|---|
| Kulinda udhibiti wa kidemokrasia wa mwanachama | Bodi zichaguliwe na wanachama wa ushirika. Serikali haipaswi kushikilia mamlaka ya kuchagua au kuidhinisha wajumbe wa bodi | Wajumbe wa bodi watawajibika kwa wanachama walio wachagua, sio kwa serikali au kikundi kingine kutoka nje ya ushirika. |

**Mfano Wezeshi:** **Mfumo wa Kanuni za Ushirika ξ 38, 1990 za Filipino:** Usimamizi wa shughuri za ushirika utakuwa chini ya bodi ya wakurugenzi "waliochaguliwa na mkutano mkuu kwa muda uliowekwa na sheria ndogondogo."

**Mfano usio Wezeshi:** **Sheria ξ 127, 2003 ya Vyama vya Ushirika ya Tanzania:** Msajili kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii anaweza kuwateua wajumbe maalum kwenye bodi ya chama chochote kilichosajiliwa katika kupokea msaada wa fedha kutoka serikalini au kama Msajili ataona uteuzi huo unafaa kwa manufaa ya umma au manufaa ya Chama."

| | | |
|---|---|---|
| Kulinda uhuru | Sheria ndogondogo zitaamua ukubwa na muundo wa bodi. Sheria haipaswi kuagiza matumizi ya mafungu au vigezo maalum vingine vya kuchagua bodi ya wakurugenzi kupita kiwango cha chini cha utoaji uamuzi (k.v. wajumbe watatu au zaidi | Ukubwa na muundo unaofaa wa bodi ya wakurugenzi utategemea ukubwa wa ushirika, nyanja husika, na uwezo wa kiutendaji |

**Mfano Wezeshi:** **Rasimu ya Sheria ξ 31 (4), 2001 ya Vyama vya Ushirika ya Jamhuri ya Czech:** Wajumbe wa Bodi watachaguliwa kulingana na idadi iliyotajwa na sheria ndogondogo, hata hivyo Bodi itakuwa na angalau wajumbe watatu.

**Mfano usio Wezeshi: Sheria ξ 63 (1), 2003 ya Vyama vya Ushirika ya Tanzania:** "Kila Bodi na Chama kilichosajiliwa itajumuisha wajumbe wasiopungua watano na sio zaidi ya wajumbe tisa.

## 8. Hesabu za Mtaji

| Kanuni Kuu | Utekelezaji wa Kanuni Kuu | Sababu za Msingi |
|---|---|---|
| Zinahitaji ushiriki wa mwanachama kiuchumi | Kugawanya kulingana na kiwango cha ushiriki. Ugawanyaji wa ziada ya ushirika utahitajika kugawiwa kulingana na ushiriki wa ushirika na si kwa kiwango cha mtaji uliowekezwa | Ugawanyaji kwa kuzingatia ulezi unatokana na kanuni za mapayonia wa Rochdale ambao waliiona kanuni hiyo kama njia ya kutuza uaminifu kulipa faida kubwa kwa wanachama walaji na kutofautisha shughuli zao na mtaji wa vyama vya ushirika. Inasemwa kuwa Vyama vya ushirika ni jumuiya za watu, sio mtaji. |

**Mfano Wezeshi: Wisconsia, U.S.A., Wis Sat ξ 185 (3), 2004:** Baada ya kuondoa gharama za uendeshaji, kiasi kinachobakia kisijumuishwe kwenye mapato ya ushirika, bali kigawanywe na kulipwa kwa walezi kulingana na uwiano ambao mteja anastahili kupata kulingana na wateja wote.

| | | |
|---|---|---|
| Kulinda udhibiti wa kidemokrasia wa mwanachama | Kuruhusu mifuko ya akiba na mtaji. Sheria isiamuru ugawanyaji kama ule ambao ushirika usingechagua kuweka mfuko wa akiba au mtaji kwa vitegauchumi vya biashara, wala kuamuru kiasi fulani cha mgawanyo kwenda kwenye fungu hilo | Kutengeneza mifuko ya akiba na mtaji kwa ajili ya vitegauchumi vya siku zijazo ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza na kukuza biashara yeyote. Kiasi ambacho kinafaa kukiweka kwenye mfuko wa akiba kitatofautiana kulingana na biashara. |

**Mfano Wezeshi: Wisconsini, Merekani, Wis, Stat ξ 185.45 (4) (a), 2004:** "Mapato yeyote halisi ya ziada yanaweza kuingizwa kwenye au akiba ya ushirika iliyogawiwa au ambayo haijagawiwa."

**Mfano Usio Wezeshi: Sheria ξ 33,2003 ya Vyama vya Ushirika ya Sudani:** "Chama kitaanzisha mfuko wa akiba na kila mwaka kitahamishia humo angalau asilimia 25 ya faida."

## 9. Ukaguzi wa Hesabu

| Kanuni Kuu | Ukamilishaji wa Kanuni Kuu | Kanuni za Msingi |
|---|---|---|
| Kulinda Udhibiti wa Kidemokrasia wa Mwanachama<br><br>Kulinda uhuru | Uchaguzi kufanywa na wanachama: Wanachama wa ushirika wanapaswa kuwa na haki ya kumchagua mkaguzi wa hesabu wanayemtaka. | Madhumuni ya ukaguzi wa hesabu ni kuwezesha udhibiti wa wanachama wa ushirika kwa kuhakikisha kwamba shughuli zinafanywa kwa uaminifu na kwa utaalamu |

**Mfano Wezeshi:** **Sheria ξ 18,2003 ya Ushirika ya Ukraine:** Mkaguzi wa hesabu anaripoti kwenye mkutano mkuu wa ushirika na atachaguliwa na mkutano mkuu miongoni mwa wanachama wa chama cha ushirika kulingana na taratibu za upigaji kura ambazo zinawekwa na sheria za ushirika."

**Mfano Usio Wezeshi:** **Sheria ξ 140-41, 1970 ya Vyama vya Ushirika ya Zambia:** Msajili anapewa mamlaka ya kukagua hesabu, au kuchagua mtu mwingine kuwa mkaguzi wa hesabu.

## 10. Kusuluhisha Migogoro

| Kanuni Kuu | Utekelezaji wa Kanuni | Kanuni za Msingi |
|---|---|---|
| Kuepuka migongano ya Wajibati<br><br>Kutoa Mfumo ulio wazi na unaofaa wa kikanuni<br><br>Kulinda mchakato unaostahili | Kuwepo kwa mahakama na majukwaa ya kimila yaliyo huru. Chombo chochote kulichokabidhiwa jukumu la kuamua migogoro ambayo inavihusu vyama vya ushirika vinapaswa kuwa huru na kisichojihusisha na uhamasishaji, usimamizi na majukumu mengine ya mipango ya ushirika. Vyama vya ushirika viwe huru kutumia mahakama mbalimbali, pamoja na kujitolea kuwa na makubaliano ya usuluhishi. | Taratibu za migogoro lazima ziwe hazina upendeleo na zifuate haki na wala zisiwahusishe viongozi ambao wana majukumu mengine yahusuyo kuendeleza au kurekebisha vyama vya ushirika. Taratibu zinazotumika katika utoaji maamuzi na usuluhishaji kwa ajili ya shughuli nyingine zikitumika zinaweza kupunguza mwingiliano wa kazi. |

**Mfano Wezeshi:** **Sheria ξ 82, 1992 ya Vyama vya Ushirika ya Malaysia:"** Migogoro yote inayohusu vyama vya ushirika itapelekwa kwa Msajili Mkuu kwa ajili ya kutolewa uamuzi."

## 11. Uvunjikaji/umalingamisho/Muungano

| Kanuni Kuu | Utekelezaji wa Kanuni Kuu | Sababu za Msingi |
|---|---|---|
| Kuheshimu uwanachama wa hiari<br><br>Kulinda mchakato | Taratibu kwa ajili ya idhini ya wanachama. Sheria inapaswa kutoa taratibu kwa ajili ya kubadilisha au kuvunja chama, yakiwemo mahitaji ya akidi na upigaji kura, taratibu za utoaji | Vyama vya ushirika ni vyama vya hiari, vinavyohusisha uwezo wa kubadilisha au kujitoa, pamoja na kuundwa kwa uamuzi wa wanachama |

| | | |
|---|---|---|
| unaostahili | taarifa kwa wanachama, kuruhusu kujitoa, na kugawanya raslimali zinazobakia baada ya kuvunja chama. | |

Mfano Wezeshi: **Sheria ξ 90, 1989 ya Vyama vya Ushirika ya Botswana**: Taarifa kuhusu haki za wanachama kuhusiana na uamuzi wa umalingamisho "itatumiwa kwa wanachama wowote na wadai" na mwanachama yeyote "kwa taarifa ya maandishi (anaweza) kugusia nia yake ya kutokuwa mwanachama wa chama kilichomalingamishwa."

Mfano Usio Wezeshi: **Sheria Na. 1-164, 1993 ya Ushirika ya Lithuania:** Haionyeshi chochote kuhusu umalingamisho, muungano, au mgawanyiko.

### 12. Ushirika wa vyama vya ushirika (Apex)

| **Kanuni Kuu** | **Kutekeleza Kanuni Kuu** | **Sababu za Msingi** |
|---|---|---|
| Kulinda uhuru na uwezo wa kufanya maamuzi pasipo kuingiliwa | Uhuru unaoruhusiwa. Sheria inapaswa kuruhusu kuundwa kwa jumuiya za muungano wa vyama vya ushirika kama vile muungano, shirikisho na muungano wa shirikisho, bila kutoa amri kuhusu muundo uweje au kuvitaka vyama vya ushirika kuunda au kusaidia vyama hivyo | Utoaji wa huduma kupitia muungano wa vyama vya ushirika vya kati (apex) kutaimarisha hali ya kidemokrasia na utaalamu halisi wa umoja wa ushirika. Kuamuru muundo wa vyama vya ushirika kunapoteza uhuru wa kidemokrasia wa kila ushirika na kunaweza kuendeleza hali ya kutokuwa na ufanisi ambayo itazuia ushindani. |

Mfano Wezeshi: **Kanuni ξ 1, 1990 ya Ushirika ya Ufilipino.** "Serikali inatambua haki za sekta ya ushirika ya kuanzisha na kuendeleza huduma za ushirika ikiwa ni pamoja na kutangaza, kuhamasisha, kupanga, mafunzo, ukusanyaji taarifa, ukaguzi wa hesabu na misaada."

Mfano usio Wezeshi: **Sheria ξ 17,2003** ya Vyama vya Ushirika ya Tanzania: Inamruhusu msajili wa vyama vya ushirika kuvitaka vyama vyovyote viwili au zaidi kuunda na kuomba usajili wa chama cha ushirika."

## KANUNI ZA KUSHIRIKI KWENYE SEKTA- USHIRIKA YA KISHERIA NA UDHIBITI

### 1. Kushiriki kwenye Sekta

| Kanuni Kuu | Utekelezaji wa Kanuni Kuu | Sababu za Msingi |
|---|---|---|
| Kukuza Upatikanaji wa masoko na usawa wa huduma | Kuondoa mahitaji ya aina fulani ya ushirika. Kanuni mahsusi za sekta hazipaswi kutoa amri kuhusu aina ya ushirika wa biashara kwa namna ambayo itaondoa ushiriki katika ushirika | Shughuli za ushirika zinaweza na zinapaswa kuruhusiwa kufanywa katika sekta yoyote ya uchumi. |

**Mfano Wezeshi:** **Shirika la Kazi Duniani Rec. Na. 193 ξ 7 (2), 2002:** Vyama vya ushirika vinapaswa kutendewa kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa nchi kwa namna ambayo upendeleo utakuwa sawa na ule wa makampuni na mashirika mengine ya kijamii."

**Mfano usio Wezeshi:** Honduras: Sheria zinataka makampuni ya bima yawe makampuni ya hisa, kiufanisi kuzuia kujiunga katika ushirika.

| | | |
|---|---|---|
| Kukuza upatikanaji wa masoko bila kupingwa<br><br>Kukuza kanuni za haki | Uingizaji wa masharti ya yaliyo katika Makampuni. Mifumo ya kikanuni ya ushirika inapaswa kuepuka masharti magumu, yakijumuisha masharti ya akiba ya mtaji kwenye tasnia ya benki na bima ambayo yamepangwa kwa ajili ya biashara kubwa | Kwa kawaida vyama vya ushirika vinahudumia wananchi ambao kiwango cha huduma wanachokipata kutoka kwenye shughuli za mwanzo ni hafifu, wakiwemo wananchi maskini au waliotawanyika ambao hawayawezi masharti ya mtaji mkubwa au kukidhi masharti mengine ya kikanuni yaliyowekwa kwa ajili ya biashara kubwa zaidi. |

**Mfano Wezeshi:** **Baraza la Dunia la Vyama vya Kukopa, inc. Sheria ya Chama cha Kukopa cha Kielezo, 2005**: Mtaji wa kitaasisi wa chama cha kukopa, unapaswa kuwekwa katika kiwango cha chini cha asilimia 10 kuhusiana na raslimali za chama cha kukopa zilizokadiriwa na bima."

**Mfano usio Wezeshi:** **Peru:** Kanuni za bima zinaweka masharti ya mtaji mikubwa ambayo inazuia kuundwa kwa vyama vidogo vya ushirika vya bima ambavyo viko katika nchi nyingine nyingi.

### 2. Uunganishaji

| Kanuni kuu | Utekelezaji wa Kanuni kuu | Sababu za msingi |
|---|---|---|
| Kukuza upatikanaji wa masoko<br><br>Kulinda mchakato unaostahili | Haki ya kujiunganisha kwenye viwango visivyo vya kibaguzi. Katika tasnia ya miundombinu, kama vile mawasiliano ya simu na umeme, wanaojiunga wapya lazima wawe na haki ya kuunganishwa kwenye mfumo wa wagavi wanaoongoza katika viwango vilivyorekebishwa visivyo vya kibaguzi ili kuwahudumia watumiaji | Kuhodhi tasnia ya miundombinu mara nyingi kumekuwa ni kichocheo cha kukataa kushughulika na washindani au kutoa huduma kwa kiwango kisichofaa |

**Mfano Wezeshi:** **Poland, 1990:** Chini ya mfumo wa ubinafsishaji unaoruhusu makampuni mapya kushindana makampuni makubwa yaliyokuwa yakihodhiwa na serikali; vyama viwili vya ushirika (WIST na Tyczyn) vilijadiliana kuhusu taratibu za kuungana na kuchangia pamoja mapato na mgavi mkuu.

### 3. Mfumo wa Udhibiti

| Kanuni kuu | Utekelezaji wa Kanuni kuu | Sababu za msingi |
|---|---|---|
| Kuwa na mfumo wa udhibiti ulio wazi na wenye ufanisi | Fomu za utoaji taarifa zinazokubalika. Fomu za utoaji taarifa zinazokubalika zinaweza kutolewa na serikali ili kuwezesha utoaji taarifa wenye ufanisi | Hatua za udhibiti bora unaokubalika zinaipa serikali na wakopeshaji njia ya kusimamia na kuweka vigezo. |

**Mfano Wezeshi:** **Marekani**: Uongozi wa upelekaji umeme vijijini unataka kwamba vyama vya ushirika viwasilishe "Fomu na.[7]" inayokubalika kwa ajili ya kutolea taarifa kuhusu data za uendeshaji na fedha. Mbinu kama hiyo imekuwa ikitumiwa Bangladesh na Ufilipino.

| | | |
|---|---|---|
| Kuendeleza utendeaji ulio sawa | Mamlaka kuweka viwango vinavyowiana na gharama Mifumo ya kikanuni inapaswa kuruhusu vyama vya ushirika kuweka viwango vinavyotosha kulipia gharama za huduma wanazotoa, kanuni ya viwango haipaswi kupanga kiholela vipingamizi vya bei kwa kutegemea gharama za wagavi wanaopewa ruzuku au wenye gharama za chini zaidi | Vyama vya ushirika mara nyingi huhudumia maeneo ambayo ni ghali zaidi kuhudumiwa na kwa hiyo uwepo wa viwango holela cha bei kwa kutegemea gharama za Wagavi wakubwa zinaweza kuwa ni za kibaguzi zitumikapo katika ushirika. |

**Mfano Wezeshi:** **Marekani:** Mara kwa mara vyama vya ushirika husamehewa kutokana na kanuni za serikali ya viwango vya umeme kwa kutambua sifa ya kidemokrasia ya vyama vya ushirika.

### 4. Upataji Fedha

| Kanuni kuu | Utekelezaji wa Kanuni kuu | Sababu za msingi |
|---|---|---|
| Kuendeleza utendeaji ulio sawa | Vivutio vya kuhudumia maeneo ambayo hayana huduma za kutosha. Serikali inaweza kukuza maendeleo ya vyama vya ushirika kwa kutoa dhamana za mikopo au mikopo ya fedha ya moja kwa moja ya serikali ili kushusha gharama za upataji mikopo. | Bila ya dhamana za serikali au makubaliano mengine, vyama vya ushirika vinaweza kukabiliwa na gharama kubwa za mtaji katika masoko binafsi kuliko katika biashara kubwa binafsi zaidi ya hayo upatikanaji wa mtaji wa gharama ndogo unaweza kutumiwa kusaidia mfumo wa gharama za vyama vya ushirika unaohudumia maskini, jumuiya zilizotawanyika au zilizo mbali na maeneo yenye huduma ambazo ni gharama kubwa kuzihudumia. |

**Mfano Wezeshi:** **Marekani:** **Sheria upelekaji umeme vijijini ya Marekani ya 1936:** Vyama vya Ushirika vinapewa fursa kupata ruzuku ya mikopo ya gharama ndogo na upendeleo wa kupata vyanzo vya umeme vya gharama ndogo vinavyomilikiwa na serikali.

## 5. Utozaji Kodi

| Kanuni kuu | Utekelezaji wa Kanuni kuu | Sababu za msingi |
|---|---|---|
| Kuendeleza usawa katika kuhudumiwa | Kutofautisha baina ya miamala ya wanachama na ile ya wasio wanachama.<br><br>Ziada inayogawanywa kwa uwiano kwa mteja wa mwanachama wa ushirika isamehewe kodi. Mapato yanayotokana na miamala ya wasio wanachama yanaweza yakatozwa kodi kama ilivyo kwa mashirika mengine | Ziada inayogawanywa kwa uwiano wa mteja wa ushirika sio faida bali inalipwa kutoka kwenye gharama za ziada. Kama Ushirika unafanya shughuli na wasio wanachama na kutoza zaidi ya gharama zake, mapato ya ziada, yanaweza kuchukuliwa kuwa ni faida na kutozwa kodi ipasavyo. |

**Mfano Wezeshi:** **Marekani:** Ziada halisi sio mapato yanayotozwa kodi kwa upande wa ushirika na kwa mlezi kama zinagawanywa kwa walezi kwa kuzingatia biashara iliyofanywa pamoja na ushirika.

**Mfano Usio Wezeshi: Urusi, Miaka ya 1990**: Vyama vya ushirika vinatozwa kodi kwa kuzingatia mapato yao, sio kipimo cha faida, na kwa hiyo kulemewa na viwango vikubwa sana vya kodi.

## 6. Ushindani

| Kanuni kuu | Utekelezaji wa Kanuni kuu | Sababu za msingi |
|---|---|---|
| Kuendeleza utendeaji ulio sawa | Misamaha kwa ajili ya vyama vya ushirika. Makatazo ya sheria ya ushindani kuhusu shughuli ya pamoja baina ya biashara mbalimbali yanapaswa kujumuisha misamaha kwa ajili ya vyama vya ushirika. | Sheria nyingi za ushindani zinakataza mwenendo wa pamoja unaofanywa na wafanyabiashara wanaojitegemea, kama vile kukubaliana kuhusu bei, masharti ya mauzo, na nani wa kumuuzia. Mwenendo kama kwa kawaida hufanywa na wakulima na wengine ambao wanaendesha vyama vya masoko ya ushirika, hivyo kuhitaji msamaha wa kisheria au kiufafanuzi. |

**Mfano Wezeshi:** **Sheria ya Marekani ya Capper-Volstead, 1922**: Inatoa misamaha inayodhibiti uhodhi wenye ukomo kwa ajili ya vyama vya masoko ya ushirika ambavyo vinafuata kanuni za ushirika.

**Mfano Wezeshi:** **Kanuni ξ 8,1990 ya Ushirika ya Ufilipino:** “Hakuna ushirika au mbinu au kitendo kinachokubaliana na kanuni hii ambacho kitachukuliwa kuwa ni njama au mchanganyiko wa biashara au kuhodhi kusiko kwa kisheria.

# APPENDIX A

# APPENDIX A

## Historia fupi ya Sheria ya Ushirika na Urekebishaji kanuni katika Nchi zinazoendelea.

Kinyume na mageuzi ya juu chini ya vyama vya ushirika huko Ulaya na Amerika ya Kaskazini, ambako sheria za ushirika kwa ujumla zilifuatwa na kutambua maendeleo ya awali ya sekta ya ushirika, watawala wa kikoloni katika nchi nyingine zinazoendelea walitafuta kuendeleza vyama vya ushirika kutoka juu kwenda chini. Sheria ya ushirika katika nchi nyingi, kuanzia India mwanzoni mwa karne ya 20 na kuenea katika nchi zenye historia tofauti za kikoloni na kiitikadi zilianzisha urasimu wa kiserikali wa kulinda na kuendeleza, badala tu ya kutambua kisheria sekta ya ushirika. Uendelezaji wa vyama vya ushirika, badala yake, mara nyingi vikaunganishwa na miradi ya maendeleo ya kikoloni, Sheria za ushirika zilianzishwa "kama njia ya kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao yaliyokusudiwa kuuzwa nje, kuwaburuza wenyeji katika uchumi wa kifedha ambao ungepelekea katika utozaji kodi ulio rahisi na kuanzisha mfumo wa uchumi unaodhibitiwa kisiasa". [1]

### Maendeleo ya Ushirika Nchini India

Kuzaliwa kwa mfano wa vyama vya ushirika vilivyokuwa vikitawaliwa na serikali kunaweza kufuatiliwa katika sheria ya India ya mwaka 1904 ya Vyama vya kukopa vya Ushirika. Sheria hiyo ilizingatia bila ya kufuata sheria za vyama vya Akiba na Uzeeni na Viwanda ya Uingereza za karne ya 19, ambazo ziliweka masharti ya kisheria kwa ajili ya kuundwa kwa ushirika na kuruhusu usajili kupitia chombo cha serikali chenye utaalamu, kinachojulikana kama Msajili wa Vyama Rafiki[2]. Msajili wa vyama vya ushirika wa Uingereza alifanya kazi vilevile kama msajili wa makampuni kurekodi kuundwa kwa vyama vya ushirika, kupokea hesabu na taarifa za mwaka, na kuchunguza matumizi mabaya.[3] Lakini wajibu wa msajili wa India ulikwenda mbele zaidi, kuhudumia kama mtangazaji mwezeshaji, mrekebishaji na mshauri wa vyama vya ushirika.[4]

Lengo la kilichokuja kujulikana kama kielelezo cha sheria ya ushirika ya Classical British India lilikuwa kuhusisha serikali moja kwa moja katika kulinda umoja wa ushirika kama "mshauri rafiki"[5]. Msajili alitoa ushauri, kusaidia kutayarisha sheria ndogondogo, na kufundisha kanuni za ushirika kwa vyama vinavyoendelea, lakini vinakosa uwezo wa kutumia nguvu na kutoa adhabu.[6] Muda ulivyokuwa ukienda mbele, dhima ya msajili ilikuwa ikipungua kwa kuwa vyama vya ushirika vilivyokuwa vikiendelea vilifikia uendelevu na uwezo kiuchumi kwa ajili ya kujiongoza.

---

[1] HANS-H MUMKER & A SHAH, INT'L LABOUR OFFICE, CREATING A FAVOURABLE CLIMATE AND CONDITIONS FOR COOPERATIVE DEVELOPMENT IN AFRICA. Working Paper 7 (1993); see also HANS-H MUNKNER. General Report in COMPARATIVE STUDY OF THE RELEVANT LAW ON COOPEATIVE SOCIETIES AND OTHER SELF-HELF ORGANIZATIONS IN AFRICA 26 (1986) Kuelezea kuanzishwa kwa vyama vya ushirika "kupambana dhidi ya matatizo ya kijamii kama vile wakulima kuwategemea wafanyabiashara wa wakopeshaji pesa na kueneza mifumo ya maadili na taratibu za mwenendo mabwana wakoloni miongoni mwa wenyeji (uzoeaji wa utamaduni.)"

[2] RITA RHODES, Colonial Co-operatives through the eyes of their Cooperative Registrars, in 100 YEARS CO-OPERATIVE CREDIT SOCIETIES ACT.INDIA 1904,228 (Hans-H Münkner ed., 2005).

[3] *Id at 229-30*

[4] MADHAV V. MADANE, *A Centrury of Cooperative Legislation: From State Control to Autonomy to State Partnership, in* 100 YEARS CO-OPRATIVE CREDIT SOCIETIES ACT. **INDIA, 1904, 55-57** (Hans-H Münkner ed.2005)

[5] HANS-H MUNKER . The Classical BRITISH Indian Pattern of Cooperation. From State-Sponsorship to State Control, in 100 YEARSCO-OPERATIVE CREDIT SOCIETIES ACT, INDIA 1904 106-14 (2005)

[6] Id. at 113-14

Danieli Hamilton, mjumbe wa Kamati ya kifalme ya Kutunga Sheria ambayo ilitayarisha rasimu ya sheria ya 1904, alielezea dhima madhubuti ya serikali ya kikoloni katika maendeleo ya ushirika kama ilivyounganishwa na malengo mapana ya kikoloni ya Serikali ya "Uingereza. :Kamwe msisahau, "alielezea, "ni kuunganisha India iwe moja na hiyo kuiwezesha kuchukua nafasi yake sahihi duniani, kwamba serikali ya Uingereza ipo hapa na nyundo ya muungano iliyoko mkononi mwa serikali ni Umoja wa Ushirika."[11]

---

***Kinyume na madhumuni ya awali ya kupunguza dhima ya serikali katika maendeleo ya ushirika, utungaji wa sheria wa baadaye ulishughulikia udhaifu ulioonekana au maendeleo yaliyocheleweshwa ya sekta ya ushirika kwa kuongeza mamlaka ya msajili***

---

Kinyume na madhumuni ya awali ya kupunguza dhima ya serikali katika maendeleo ya ushirika, utungaji wa sheria wa baadaye ulishughulikia udhaifu ulioonekana au maendeleo yaliyocheleweshwa ya sekta ya ushirika kwa kuongeza mamlaka ya msajili.

Sheria ya 1925, ya Vyama vya Ushirika ya Bombay, kwa mfano, iliidhinisha serikali kushiriki katika jumla ya hisa, hivyo kuingiza serikali moja kwa moja kwenye shughuli ya ushirika.[8] Sheria ya 1982 ya vyama vya ushirika ya Madras ilimpa mamlaka msajili kuchukua nafasi ya kamati ya uongozi wa ushirika kwa hiari yake.[9]

Mwelekeo wa kuongeza udhibiti wa serikali kwa vyama vya ushirika uliendelea baada ya India kupata uhuru wake. Mwaka 1955, serikali ilifadhili utafiti na kuchunguza kuwa vyama vya ushirika vya mikopo vijijini vilikuwa havikidhi mahitaji ya wakulima na ikapendekeza namna mpya ya ubia wa serikali katika vyama vya ushirika kwa ngazi tofauti."[10] Sheria zilizofuatia ziliwapa wasajili mamlaka ya kuvunja vyama vya ushirika, kuagiza kurekebishwa kwa sheria ndogondogo, kuidhinisha mikopo, kupanga uwanachama kwenye kamati ya juu zaidi ya uongozi, kuteua au kuondoa uongozi, na kuwa chombo cha kutatua migogoro ikiwa ni pamoja na migogoro inayowahusu watumishi wa ofisi ya msajili[11].

---

[11] Quoted in AKE EDEN, Oriental Economic. Thoughts and Cooperative Developemnt on the Pre-Colonial Indian Subcontment, in 100 YEARS CO-OPERAVITE CREDIT SOCIETIES ACT, INDIA 1904, 22 (Hans H.Münkner ed, 2005)

[8] MADHAV V. MADANE, A Centrury of Cooperative Legislation: From State Control to Autonomy to State Partnership in 100 YEARS CO-OPERATIVE CREDIT SOCIETIES ACT, INDIA 1904.62 (HANS-H Muünkner ed. 2005)

[9] Id at 62

[10] Id at 65

[11] Id at 66-69

## Mafanikio na Matatizo ya Mifumo ya Kisheria inayoongozwa na Serikali

Katika nchi nyingine, zilizo ndani na nje ya utawala wa kikoloni wa Waingereza, mitazamo kama hiyo ya kuongeza dhima za serikali katika udhibiti na usimamizi wa vyama vya ushirika ilifuatwa kwenye makoloni ya Uingereza, hivyo basi mtindo wa utungaji wa sheria za ushirika katika "Clasical British India" ulirudufiwa katika sehemu mbalimbali[12]. Katika makoloni ya Ufaransa, vyama vya ushirika kwa ujumla vilianzishwa kama Mashirika ya Umma na sio biashara huru.[13] Na katika nchi za kijamaa au zilizokuwa za kisovieti, vyama vya ushirika vilifanywa kuwa vyombo vya chama na serikali vilivyohusika na kutekeleza sheria kuu za mipango.[14]

Sawa na historia iliyoko India, serikali nyingi za wenyeji katika kipindi baada ya uhuru zilirekebisha sheria zao na kanuni ili kuongeza dhima ya serikali kwa vyama vya ushirika.[15] Hadi kufikia miaka ya 1960 na 1970, vipengee vya kawaida vya mifumo ya kisheria na kitaasisi katika nchi za mashariki (eastern block) na zile zilizokuwa zimepata uhuru zilijumuisha:

- Idara za ushirika kuwa na mamlaka ya kuteua na kuondoa viongozi wa menejimenti ya ushirika na kuidhinisha maamuzi ya biashara ya msingi;
- Wafanyakazi wa ushirika kutendewa sawa na watumishi wa serikali;
- Vikwazo vya kisheria kwa vyama vya ushirika kutumia mahakama, kufanya mikataba, kuchukua deni bila ya kupata idhini ya serikali.
- Vikwazo vya kisheria kwa baadhi ya michepuo ya biashara, mara nyingi viliwaondoa kwenye sekta zilizokuwa na manufaa kama vile masoko ya kilimo ya kuuza bidhaa nje;
- Vikwazo katika kuunda shirikisho ili kutoa huduma muhimu, zikiwa ni pamoja na bima, elimu, na msaada wa ukaguzi wa hesabu;
- Kuingiza vyama vya ushirika kwa mifumo rasmi ya chama cha kisiasa; na
- Uwanachama wa lazima katika vyama vya ushirika kwa wakulima au wafanyakazi wengine katika baadhi ya sekta au wakazi wa maeneo fulani/mahususi.

[12] HANS-H MUNKNER & A.SHAH.INT'L LABOUR OFFICE, Creating a Facourable Climate and Conditions for Cooperative Development in Africa 9-13 (1993); cf. KRISHAN, TAIMNI, INT'L LABOUR OFFICE, CREATING A FAVOURABLE CLIMATE AND CONDITIONS FOR COOPERATIVE DEVELOPMENT IN ASIA (1994) (discussing implementation of the Classical BRITISH Indian model in Asian countries).

[13] Id at 10-11

[14] NT'L LABOUR OFFICE, COOP BRANCH, CREATING A FAVOURABLE CLIMATE AND CONDITIONS FOR COOPERATIVE DEVELOPMENT IN CENTRAL AND EASTERN EUROPE, 17-18 (1996).

[15] See JOHN JOSEPH OGOLA, Structural Changes in COOPERATIVE Movemnets and Consequences for Cooperative Legislation in Different Countries in Affrica. Background Paper NO 1· **INT'L LABOUR OFFICE COLLOQUIUM ON STRUCTURAL CHANGES IN COOPERATIVE**

**MOVEMENTS AND CONSEQUENCES FOR COOPERATIVE LEGISLATION IN DIFFERENG REGIONS OF THE WORLS** (Ashish Shah ed 1993) karibu serikali zote za Kiafrika, baada ya uhuru, zilijiingiza katika hatua za utungaji sheria na kiuendeshaji ambazo zilivifanya vyama vya ushirika vya Kiafrika kuwa chini ya udhibiti wa serikali, na kuvishusha katika ngazi ambayo wakurugenzi na mameneja wao wana uwezo mdogo tofauti na ule walio nao mameneja wa mashirika ya umma"

Zaidi ya kuvidhoofisha vyama vya ushirika kiuchumi, vikwazo vizito kutoka serikalini. Kuhusiana na vitendo vilivyopelekea vyama vya ushirika katika nchi nyingi kupata fedheha ya kutawaliwa na serikali. Uandikaji na ushirikishaji uwanachama katika vyama vingi vya ushirika ulipungua. Ruzuku za serikali zikaongezeka maalum kwa kuhimili makampuni, kukazia bajeti za serikali.

Katika miaka ya 1980, programu za kurekebisha mifumo zilizoamriwa na Shirika la Fedha Duniani na Benki ya Dunia zilianza kulenga kwa ujumla matumizi ya serikali, na matumizi ya vyama vya ushirika. Katika nchi nyingi, ruzuku zilipopungua au kuondolewa biashara za ushirika zilikufa.

## Uendelezaji wa Kanuni za Ushirika

Kuenea kwa haraka kwa shughuli za ushirika huko Ulaya na Amerika ya Kaskazini katika miaka ya kati ya 1800 kwa sehemu kumesifiwa kutokana na kuundwa na kusambazwa kwa kanuni za ushirika kulikofanywa na British Rochdale Society of Eauitable Pioneers na Ushirika wa kuweka na kukopa wa German Raiffeisen. Kanuni zilizochapishwa na Rochdale Society miaka ya 1840 kuelekea 1860 zilikuwa na athari kubwa.

Chama cha Rochdale kilianzishwa na wafuma fulana 28 mwaka 1844 kama ushirika wa walaji. Waasisi wa Chama cha Rochdale ambao kila mmoja alichangia ₤ 1 ya kununulia bidhaa kwa jumla za kuuzwa kwa wanachama bila ya kuweka faida. Chama kilivyokuwa kikiendelea, kiliongeza kiwango chake na kuuza bidhaa kwa bei ya kawaida ya rejareja, ambapo faida iligawanywa miongoni mwa wanachama kwa uwiano kulingana na kiasi kilichotumiwa katika ununuzi kwa mwaka. Kanuni zinazoongoza shughuli za Chama cha Rochdale baadaye kilikuja kujulikana kama Kanuni za Rchdale, ambazo baadaye zilitumika kuanzisha vyama vingine vya ushirika vya Walaji Uingereza yote na kwingineko [16] Tofauti kuhusiana na Kanuni za Rochdale zilitumiwa na vyama vya ushirika vya kitaifa na kimataifa duniani kote, ikiwa ni pamoja na Patrons of Husbandry (The Grande) wa Merekani mwaka 1876[17] na ICA mwaka wa 1937[18]. Jitihada za awali za maendeleo ya ushirika za serikali za kikoloni mara nyingi zilizingatia kanuni za Rochdale katika hali nzuri lakini juhudi zao za kufanya serikali kama kiongozi rasmi wa umoja kuliipa kanuni hii changamoto kwamba vyama vya ushirika vinategemea udhibiti wa kidemokrasia wa wanachama wake.

[16] David Thompson, Cooperative Principles Then and Now, 53 Coop Grocer (July-Aug 1994), available at www.cooperativegrocer,coop/articles/index.php?id=158

[17] JAMES R. BAARDA, COOPERAVITE PRINCIPLES AND STATUES LEGAL DESCRIPTIONS OF UNIQUE ENTERPRISES U.S Dep't of Agric.AGRIC,COOP SERV.RESEARCH REP. NO. 54 (1986)

[18] 18 See INT'L CO-OP.INFO. CTR.PRINCIPLES, available at www.wisc.edu/uwcc/icic/def-hist/gen-info/.

## Kanuni za Rochdale za Shughuli ya Ushirika

**Uwanachama wa wazi:**
Ushirika ulimruhusu kila mmoja kujiunga na kwa mwanachama mpya kabisa kulipa ada ya kiingilio kama mwanachama wa zamani:

**Udhibiti wa kidemokrasia (mtu mmoja kura moja)**
Upigaji kura ulizingatia kanuni ya Chartism ya mtu mmoja kura moja, bila ya kujali idadi ya hisa alizomiliki kila mtu.

**Ugawaji wa ziada kulingana na biashara.** Ili kutuza uaminifu na kurejesha faida kwa wanachama walaji, ziada iligawanywa kulingana na biashara na ushirika katika maslahi ya umiliki.

**Ulipaji wa riba ndogo kwenye mtaji**
Kwa kulipa kiwango cha riba kilichopangwa kuliko cha kubahatisha, chama kinaweza kutumia ziada ya nyongeza kutoa mishahara mizuri zaidi na hali bora za kazi, na kuendeleza utoaji tuzo. Hisa katika ushirika zilitunzwa kwa thamani, kuliko kuamuliwa katika soko.

**Kutofungamana kisiasa na kidini**
Rochodale Society iliongeza kanuni hii kwa kuona uzoefu wa baadhi ya vyama vya ushirika vilivyokuwa na ufadhili wa kisiasa ambavyo mara kwa mara vilisusiwa na vikundi vya walaji wakipinga misimamo yao iliyokuwa na utata.

**Biashara ya fedha**
Moja ya sababu kubwa za kushindwa kwa vyama vya ushirika vya awali ilikuwa ni kutoa mikopo kwa wanachama, ambayo ilihitaji kupandisha bei ili kufidia hasara.

**Kuendeleza elimu:**
Baada ya msajili kuruhusu vyama vya ushirika kutenga fedha kwa ajili ya elimu, kanuni hii iliongezwa, ambapo hapo awali, vyama vya ushirika vilitenga isivyo halali fedha kwa ajili ya elimu.

## Pendekezo 127(1966) la ILO, Sehemu III. A Utungaji Sheria

10. Hatua zote zinazofaa, zikiwa ni pamoja na kushauri vyama vya ushirika vilivyopo, zinapaswa kuchukuliwa
    a. Kugundua na kuondoa masharti yaliyomo kwenye sheria na kanuni ambayo yanaweza kuwa na athari ya kuzuia maendeleo ya vyama vya ushirika kupitia ubaguzi, kwa mfano kuhusiana na utozaji kodi au utoaji wa leseni na mafungu, ama kwa kushindwa kuzingatia sifa maalum za vyama vya ushirika au za kanuni mahsusi za uendeshaji wa vyama vya ushirika.
    b. Kuepuka kuingizwa kwa masharti hayo kwenye sheria za kanuni za baadaye
    c. Kutumia sheria na kanuni za kihazina kwa masharti maalum ya vyama vya ushirika.

11. Kunapaswa kuwepo na sheria au kanuni zinazohusika mahususi na kuanzishwa na utendaji wa vyama vya ushirika na kwa ulinzi wa haki zao kufanya kazi kwa masharti yaliyo chini tofauti na aina nyingine za sheria au kanuni hizi zitumiwe hasa kwa aina zote za vyama vya ushirika.

12.1 Sheria na kanuni hizi zinapaswa kwa namna yoyote ile zijumuishe masharti kuhusiana na masuala yafuatayo.
    a. Ufafanuzi au maelezo ya ushirika kuelezea sifa zake muhimu, ambazo ni chama cha watu ambao wamejitolea kuungana pamoja kufikia lengo la pamoja kupitia kuunda chama kinachodhibitiwa kidemokrasia, kutoa michango iliyo sawa katika mtaji unaohitajika na kukubali hisa sawa, hatari na faida za shughuli ambazo wanachama wanashiriki kikamilifu.
    b. Maelezo ya malengo ya ushirika, na taratibu za kuanzishwa kwake, usajili, marekebisho ya sheria zake na kuvunjika kwake.
    c. Masharti ya wanachama, kama ile kiwango cha juu kwa kila hisa ,na kila itakapofaa, uwiano wa hisa zinazotakiwa wakati wa michango na muda unaoruhusiwa kutoa malipo kamili, pamoja na haki na majukumu ya wanachama, ambayo yataelekezwa kwa kina kwenye sheria ndogondogo za vyama vya ushirika.
    d. Mbinu za uongozi, usimamizi na ukaguzi wa hesabu wa ndani na taratibu kwa ajili ya kuanzishwa na utendaji wa vyombo husika
    e. Kulinda jina "Ushirika"
    f. Taratibu kwa ajili ya ukaguzi wa nje na mwongozo wa vyama vya ushirika na kwa ajili ya utekelezaji wa sheria na kanuni

2. Taratibu zilizoonyeshwa kwenye sheria au kanuni hizo, hususan taratibu za usajili, zinapaswa kuwa rahisi na zinazotekelezeka kwa jinsi iwezekanavyo, ili zisizuie kuanzishwa na maendeleo ya vyama vya ushirika.

13. Sheria na kanuni inazohusu vyama vya ushirika zinapaswa ziidhinishe vyama vya ushirika kuungana kuwa shirikisho.

Katika Mwaka 1966, ICA ilitofautisha baina ya kanuni zinazotumika kuwa vyama vya ushirika kamili ICA ilielezea kwamba demokrasia katika uongozi wa vyama vya ushirika inamaanisha kujitegemea kwa maana ya uhuru wa udhibiti wa nje. [19]" Lakini katika nchi zinazoendelea, "ICA ilihitimisha kwamba" watu ambao ndio kwanza wanaanza kujifunza ushirika wakati wote hawajajiandaa kiasi cha kutosha kusimamia vyama vya ushirika kwa mafanikio[20]. "Hivyo ripoti ilihitimisha kwamba serikali katika nchi zinazoendelea zinaweza "kusisitiza" kwamba ushauri wa kitaalamu unaofaa unazingatiwa," ikiwa ni pamoja na kuwataka wawakilishi wake wakae kwenye uongozi kwa wakati,"[21]

Katika mwaka huohuo, Shirika la Kazi Duniani (ILO) lilipitisha Pendekezo 127 kuhusu na dhima ya vyama vya ushirika katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi zinazoendelea.[22] Ingawa pendekezo linatoa seti inayofaa ya kanuni za mageuzi ya kisheria, sehemu ya "Msaada wa Uendeshaji iliidhinisha mamlaka za usimamizi za ushirika kwa ajili ya kipindi cha mwanzo tu," pamoja na aina ya uwezo wa kuteua wafanyakazi wa ushirika na kutoa maelekezo na ushauri "ambavyo vilitumiwa kutawala vyama vya ushirika katika nchi nyingi zinazoendelea.

Matatizo yaliyovikabili vyama vya ushirika vilivyotawaliwa na serikali miaka ya 1970 na 1980 yaliharakisha uchunguzi mwingine wa dhima ya serikali katika maendeleo ya ushirika.[23] Mwaka 1995, ICA ilipitisha Tamko Jipya kuhusu utambulisho wa Ushirika ambao unatumika sawa kwa vyama vyote vya ushirika, na kusisitiza umuhimu wa kutambua vyama vyote vya ushirika kama shughuli huru, zisizosimamiwa na serikali.[24] Hivi karibuni ILO ilianzisha mchakato wa miaka mingi wa kuangalia upya Pendekezo 127, kutokana na kupitishwa Pendekezo 193 mwaka 2002. Pendekezo 193 linaondoa idhini ya awali ya uongozi kuingilia masuala ya ushirika na kuitisha Tamko la ICA kuhusu utambulisho wa Ushirika kama unavyotumika kwa vyama vyote vya Ushirika.[25.]

---

[19] INT'L COOP.INFO.CTR., Report of the ICA Commission on Co-operative Principles (1966), availabe at www.wisc.edu/uwcc/icic/def-hist/gen-inro/Report-of -the-ICA-Commision-on-Co-opera-1/index.html

[20] Id (explaining that "it must be recognised that, in co-operatives which are themselves at the beginning of their development, their democratic organs also are very probably underdeveloped and likewise, the capacity of their members for carrying out democratic procedures efficiently and for submitting readily to democratic discipline.")

[21] *Id*

[22] INT'L LABOUR OFFICE, RECOMMENDATION 127: THE ROLE OF COOPERATIVES IN THE ECONOMIC AND SOCIIAL DEVELOPMENT IN DEVELOPING COUNTRIES (1996).

[23] See ALFRED HANEL STATE-SPONSORED COOPERATIVES AND SELF-RELIENCE SOME ASPECTS OF THE REORGANIZATION OF OFFICIALIZED COOPERATIVE STRUCTURES WITH REGARD TO AFRICA (1989): HANS-H MÜNKNER, African Co-operatives and the State in the 1990s, in YEARBOOK OF COOP.ENTER 91982): INT'L LABOUR OFFICE, THE RELATIONSHIP BETWEEN THE STATE AND COOPERATIVE IN COOPERATIVE LEGISLATION REPORT OF A COLLOQUIUM HELD AT GENEVA, 24-15 Dec 1993 (1994): SANJEEV CHOPRA, CTR. FOR CO-OPS & RURAL DEV. CO-OPERATIVES FROM CONTROLS TO A REGULATORY FRAMEWORK: POLICIES FOR THE SAARC REGION (Book World 1999).

[24] INT'L COOP. ALLIANCE, STATEMENT ON COPERATIVE IDENTITY (1996)

[25] INT'L LABOUR OFFICE, RECOMMENDATION 193: RECOMMENDATION CONCERNING THE PROMOTION OF COOPERATIVES (2002)

## Tamko la ICA kuhusu utambulisho wa Ushirika (1996)

**UFAFANUZI:** Ushirika ni chama huru cha watu wanaojiunga kwa hiari yao kukidhi mahitaji yao ya pamoja ya kiuchumi; kijamii na kiutamaduni na matamanio kupitia shughuli ya umiliki wa pamoja yanayodhibitiwa kidemokrasia

**MAADILI:** Vyama vya ushirika vinazingatia maadili ya kujisaidia wenyewe, uwajibikaji binafsi, demokrasia, usawa, haki na mshikamano. Katika utamaduni wa waasisi wake, wanachama wa vyama vya ushirika wanaamini katika maadili ya uaminifu, uwazi, uwajibikaji kijamii na kujali wengine.

**KANUNI:** Kanuni za ushirika ni miongozo ambayo vyama vya ushirika huweka maadili yake katika vitendo

1. **Uwanachama wa kujitolea na uwazi:** Vyama vya ushirika ni vyama vya kujitolea, vilivyo wazi kwa watu wote wanaoweza kutumia huduma zao na kuwa tayari kukubali majukumu ya uwanachama bila ya ubaguzi wa kijinsia, kijamii, rangi, kisiasa na kidini.

2. **Udhibiti wa kidemokrasia wa Mwanachama:** Vyama vya ushirika ni vyama vya kidemokrasia vinavyodhibitiwa na wanachama wake, ambao hushiriki kikamilifu katika kuunda sera zao na kufanya maamuzi. Wanaume na wanawake wanaotumika kama wawakilishi wa kuchaguliwa wanawajibika kwa uwanachama. Katika vyama vya msingi wanachama wana haki za kura sawa (mwanachama mmoja, kura moja), na vyama vya ushirika katika ngazi nyingine huongozwa kwa namna ya kidemokrasia.

3. **Ushiriki wa Mwanachama kiuchumi.** Wanachama huchangia kwa usawa na kudhibiti kidemokrasia mtaji wa ushirika wao. Angalau sehemu ya mtaji kwa kawaida ni mali ya pamoja ya ushirika. Kwa kawaida wanachama hupata fidia ndogo, kama itakuwepo, kuhusu mtaji uliotajwa likiwa ni sharti la uwanachama. Wanachama hutenga ziada kwa ajili ya baadhi ya madhumuni yote yafutayo: kuendeleza ushirika wao, ikiwezekana kwa kuweka akiba, ambayo sehemu yake angalau itakuwa haigawanyiki, kuwanufaisha wanachama kwa uwiano wa miamala yao na ushirika, na kuunga mkono shughuli nyingine zilizoidhinisha na wanachama.

4. **Kujitawala na uhuru:** Vyama vya ushirika ni vyama vinavyojitawala, vinavyojisaidia vyenyewe na kudhibitiwa na wanachama wake. Kama vikiingia kwenye makubaliano na vyama vingine, zikiwemo serikali, au kupata mtaji kutoka katika vyanzo vya nje, vinafanya hivyo kwa masharti kwamba vinahakikisha upo udhibiti wa kidemokrasia wa wanachama wake na kudumisha uhuru wa ushirika.

5. **Elimu, Mafunzo na Habari:** Vyama vya Ushirika vinatoa elimu na mafunzo kwa wanachama wake, wawakilishi wa kuchaguliwa, mameneja na wafanyakazi ili waweze kuchangia kwa ufanisi katika maendeleo ya vyama vyao vya ushirika. Vinaufahamisha umma hususan vijana na viongozi – kuhusu hali na manufaa ya Ushirika.

6. **Ushirikiano Miongoni mwa Vyama vya Ushirika:** Vyama vya Ushirika vinahudumia wanachama wake kwa ufanisi na kuimarisha ushirika kwa kufanya kazi pamoja kupitia mifumo ya kieneo, kitaifa, kikanda na kimataifa.

7. **Shauku ya Ujumuifu:** Ushirika unafanya kazi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya jamii zao kupitia sera zilizoidhinishwa na wanachama wake.

Hivi leo, kuna makubaliano mapya miongoni mwa vyama vya ushirika na wataalamu wa maendeleo ambayo yanakataa viwango tofauti vya sheria za vyama vya ushirika katika nchi zinazoendelea na kuidhinisha kwa uthabiti kujitawala kwa vyama vyote vya ushirika kutoka kwenye udhibiti wa Serikali[26]. CLARITY imetokana na makubaliano na madhumuni ya kusukuma mbele mawazo katika utekelezaji